OFISI YA RAIS– TAMISEMI.
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
SHULE YA SEKONDARI BWIRU WAVULANA

S.L.P 217,
MWANZA
25/03/2022.

Email – bwiruboyssecondaryschool1920@gmail.com
Website – http://bwiruboystech.sc.tz
Mkuu wa shule. 0626 245451/0756393206
Makamu mkuu wa shule. 0769 027600/0620 437834.
Patroni 0757903745/0674246586.
Mtaaluma. 0755704903/0789701777.

MZAZI/MLEZI WA……
S.L.P…….
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI BWIRU WAVULANA KIDATO CHA TANO 2022/2023. HALMASHAURI YA ILEMELA MKOA WA MWANZA

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Tano katika shule hii** mwaka **2022/2023 Tahasusi ya PCB, PCM na EGM** Shule ya Sekondari ya Ufundi Bwiru Wavulana ipo umbali wa kilometa 8 kutoka katikati ya jiji la Mwanza. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha Daladala **NATA**. Nauli ya Daladala toka stendi ya **NATA** hadi shuleni ni Tsh. 500. shule ipo mwisho kabisa zinapogeuzia gari.

Muhula wa masomo unaanza tarehe --------, hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ----------.

Fika shuleni kwa tarehe iliyopangwa na **FOMU** hii ikiwa imejazwa.. Hakuna sababu itakayokubalika kwa yeyote kutofika shuleni mapema. Hali kadhalika jiepushe na aibu ya kuumbuka kwa kuja shuleni kwa jina la mtu mwingine.

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE:

A1: KARO.

Ada ya shule shilingi **70,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa awamu mbili shilingi **35,000/=** kila mwanzo wa muhula. Fedha zilipwe kwenye A/C ya shule Na. **31101200165** Benki ya **NMB,** jina la akaunti Shule ya sekondari ya ufundi **Bwiru**. (**Hatupokei pesa taslimu**), mwanafunzi aje na stakabadhi ya Benki. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

A2: Fedha zote zilizoainishwa kwenye jedwali lifuatalo zilipwe kwenye account ya shule namba **31106600182** benki ya **NMB.** Jina la account Elimu ya kujitegemea **Bwiru Wavulana.**

Taaluma	20,000/=
Ulinzi	10,000/=
Ukarabati wa samani	15,000/=
Afya	20,000/=
Wapishi	30,000/=
Tahadhari (haitarejeshwa)	5,000/=
Kukodi godoro	10,000/=
JUMLA	**110,000/=**

A3. MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

MAHITAJI YAKUJA NAYO:

1. **VIFAA VYA TAALUMA**
   a) Rimu (bunda) mbili (02) za karatasi ya photocopy aina ya **Double A.** Mwanafunzi atatakiwa kuleta rimu moja (01) kila mwaka- Iletwe muhula wa kwanza.
   b) Madaftari saba (7) kaunta books quire four.
   c) Scientific Calculator
   d) Dissecting kit (Kwa wanafunzi wa PCB tu.)

2. **VIFAA VYA USAFI**
   Kwa wanafunzi wote **PCB,PCB** na **EGM**.
   a) Ufagio mmoja mgumu wa kufagilia nje (chelea ya wima), soft broom, Fyekeo,Jembe lenye mpini na squeezer (plastic)

3. **SARE YA SHULE**
   a) Sare ya shule hii ni suruali nyeusi (2)zisizobana zenye malinda mawili mbele na mashati meupe mikono mirefu (2)
   b) Viatu **vyeusi** vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
   c) Soksi **nyeupe** pea mbili.
   d) Mkanda wa kuvalia suruali **mweusi wa ngozi**.
   e) Sweta rangi ya **blue**.
   f) Nguo za kushindia ni suruali nyeusi na tisheti 2 za rangi ya **dark blue** zenye kola.Tisheti hizi zinapatikana shuleni.

g) Bukta **nyeusi** na raba kwa ajili ya michezo.

4. VIFAA BINAFSI

(A) chandarua na awe na utamaduni wa kukitibu kwa dawa.

(B) Vifaa vya kulia chakula, bakuli, sahani, kikombe cha uji ½ (nusu) lita, na kijiko

(C) Vifaa vya usafi binafsi kama mswaki, dawa, mafuta, toilet paper (10), Sabuni za kuogea na kufulia.

(D) tochi moja imara na betri zake.

E) godoro (futi 2 ½ kwa futi 6)

F) mashuka mawili ya rangi ya pinki ya kutandika na kujifunika, mto mmoja,foronya moja, Blanketi moja na sanduku la chuma (bati) lisiwe begi.

G) ndoo ndogo 1 yenye mfuniko.

ONYO: Hairuhusiwi kuja shuleni na nguo ambazo si sare za shule.

NB: VIFAA VIFUATAVYO VINAPATIKANA KATIKA MADUKA YALIYOPO MAENEO YA SHULE.
(mzazi anaweza kuja na pesa ili kupunguza mizigo na usumbufu).

NA	KIFAA	IDADI	GHARAMA
1	Kitambulisho na picha		6,000/=
2	Tisheti mbili zenye kola zenye nembo ya shule (rangi ya dark blue)	Pc 1	10,000/=
3	Nembo ya shule		2,000/=
4	File la mwanafunzi	Pc 1	2,000/=
5	Rimu (aina ya double A)	Pc 1	12,000/=
6	Daftari quire 4 (pc 7)	Pc 1	4,000/=
7	Sweta la shule	Pc 1	12,000/=
8	Suruali ya shule	Pc 1	15,000/=
9	Shuka (pinki) pc 2	Pc 1	8,500/=
11	Soksi nyeupe	PC1	1,000/=
13	Godoro futi $2\frac{1}{2}$ (comfy)	Pc 1	65,000/=
14	Godoro futi $2\frac{1}{2}$ (malaika)	Pc 1	35,000/=
15	Godoro futi $2\frac{1}{2}$ (deluxe)	Pc 1	45,000/=
18	Chandarua (Net)	Pc 1	6,500/=
20	Ndoo ndogo ya kuogea/kufulia	Pc 1	4,000/=
21	Dumu la lita 5 la kuhifadhia maji ya kunywa	Pc 1	2,500/=
22	Sahani, bakuli, kijiko na kikombe	Pc 4	4,000/=
23	Tochi na betri zake	Pc 1	5,000/=
24	fyekeo	PC1	5,000/=
26	Soft broom	PC1	3,000/=
27	Chelea ya wima	PC1	3,000/=
28	squeezer	PC1	3,000/=
29	Jembe lenye mpini	PC1	8,500/=

MAAGIZO MENGINE:

1. **FEDHA YA MATUMIZI:**
   Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda mjini. Mzazi ahakikishe anamnunulia kijana wake mahitaji muhimu, pia ampatie pesa kiasi kidogo kwa ajiri ya mahitaji madogo madogo ambayo hupatikana katika maduka yaliyopo hapa shuleni.

2. **FEDHA ZA MATIBABU**
   Gharama zote za matibabu zitagharamiwa na mzazi. Hivyo mzazi ampe mwanae pesa ya matibabu, au amkatie **bima ya afya.**

3. **NAULI**
   Sharti mtoto apewe nauli ya kumrudisha nyumbani kila mwisho wa mhula. Hatuna huduma ya chakula, malazi wakati shule zinapofungwa katika likizo kubwa.

4. **VYETI BANDIA VYA HOSPITALI:**
   Baadhi ya wazazi hushirikiana na watoto wao kutafuta taarifa bandia ili wasifanye kazi za shule au kula vyakula aina Fulani. Wazazi au mtoto asifanye hivyo kwa kuwa mazingira hayatamfaa kujifunza.

5. **KUJAZA FOMU:**
   Siku ya kuwasili shuleni kwa mara ya kwanza, mwanafunzi atatakiwa kuleta barua hii pamoja na fomu zilizotajwa hapo chini zikiwa zimejazwa kikamilifu.

   a) **Nyongeza na. B:**
      Fomu hii ijazwe kikamilifu na kugongwa mhuri wa Daktari wa Hospitali ya serikali ya wilaya, Mkoa au Rufaa. Taarifa ya mganga atakayejaza fomu hii itakuwa kielelezo pekee kitakachokubalika shuleni kuhusiana na afya ya mtoto. Hatupokei taarifa ya afya toka hospitali isiyo ya Serikali.

   b) **Nyongeza Na. C:**
      Historia kamili ya mwanafunzi na maelezo yake binafsi yajazwe na Mzazi/ Mlezi kwa ufasaha kwa ajili ya kumbukumbu za shule.

   c) **Nyongeza Na. D:**
      Mzazi/Mlezi aorodheshe ndugu wa karibu watakaomwona na pia atakaokwenda yeye au shule kufanya nao mawasiliano kwa niaba ya Mzazi/Mlezi.

   d) **Nyongeza Na. E:**
      Hali kadhalika, ahadi ya kutii sheria, amri na mamlaka ya shule ijazwe kikamilifu.
      Pia mwanafunzi anapofika shuleni kwa ajili ya usajili afike na nakala zifuatazo (i) nakala ya cheti cha kuzaliwa (ii) nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip) (iii) namba ya nida ya mzazi au mlezi kama anayo (iv) picha

(passport size) za Mzazi, Ndugu wa karibu au mlezi zibandikwe katika visanduku vilivyo wazi katika fomu hii, na waandike namba zao za simu Ili kurahisisha mawasiliano pindi kunauhitaji wao mfano ugonjwa, utovu wa nidhamu n.k.

MUHIMU

Fomu zote zikabidhiwe kwa mwalimu wa usajili mara tu mtoto anapowasili shuleni.

Nakutakia safari njema na karibu sana **Bwiru Wavulana.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI- (TAMISEMI)
SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI BWIRU WAVULANA
SHERIA ZA SHULE NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

NYONGEZA 'A'

1.0.UTANGULIZI:

Sheria na kanuni muhimu za shule ni mwongozo wa utaratibu wa kuishi kwa jamii iliyopo hapa shuleni ili kufanikisha maendeleo ya shule. Mafanikio ya maendeleo ya shule yanategemeana sana jinsi mwanafunzi anavyo tii na kuheshimu sheria na kanuni zilizowekwa. Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi, Tecknolojia na ufundi, yenye zamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAIS (Tamisemi) yenye majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

1.1.MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA MUDA WOTE.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni (preparation):

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na

(i) Kutunza mali za umma

1.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MARA MOJA.

(1) Wizi
(2) Kutokuhudhuriamasomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
(3) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(4) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
(5) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
(6) Kufuga ndevu
(7) Uleviau unywaji wa pombe na matumizi ya madawa kulevya
(8) Uvutaji wa Sigara
(9) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
(10) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(11) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi
(12) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(13) Kutembea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(14) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(15) Kudharau bendera ya Taifa
(16) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(17) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KIAMBATANISHO NYONGEZA B

MEDICAL EXAMINATION FORM DATE ……

NAME OF STUDENT ……

Tomedical officer I/C of…… District/Regional/Referal Designated Hospital, P.O.BOX ……..
Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two year of Secondary school education. The examination should include categories a – p. In case of an acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligble of admission to schools of students with special needs.

(a) Eye sight ……..
(b) Heart examination……
(c) Blood pressure…….
(d) Chest X-Ray ……
(e) Hearing…….
(f) Speech……..
(g) Venereal Disease …….
(h) Leprosy …….
(i) Epilepsy ……
(j) Stool routine ……C/S……
(k) Urine routine……C/S……
(l) Sickle cell test …….
(m) WBC total Differential……..
(n) OBP including ESR…….
(o) FOB……B/S……..
(p) Others ……

NAME…….. SIGNATURE…….

DESIGNATION…….

OFFICIAL STAMP……. DATE……

KIAMBATANISHO NYONGEZA C.

Bandika picha moja ya mwanafunzi hapa, Awe na shati jeupe la shule.

HISTORIA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:

1.MAELEZO BINAFSI:

(a) Jina la mwanafunzi ……..
(b) Majina ya wazazi i) Baba …… Hai/amefariki.
ii) Mama ……Hai/amefariki.
(c) Kabila la mwanafunzi ……
(d) Tarehe ya kuzaliwa (mwanafunzi)…… mkoa …….
Wilaya …… Tarafa ……Kata ……..
Kijiji ……. alikozaliwa
(e) Ni raia wa ……
(f) Jina la mlezi (kama anatunzwa na mlezi) ……..
(g) Uhusiano na mlezi …….
(h) Kazi ya mzazi/mlezi …….
(i) Ni wa ngapi kuzaliwa katika familia …… afya yake kwa ujumla ……..
(j) Matatizo maalumu aliyonayo mwanafunzi ……..

2**: SHULE ALIZOSOMA**.

Na.	**SHULE**	**WILAYA/NCHI**	**MADARASA**	**MWAKA WA KUANZA NA KUMALIZA**	
1.					
2.					
3.					
4.					

3: MAELEZO YA NYONGEZA KAMA YAPO.

……

Saini ya Mwanafunzi …… Tarehe …….

4: **KUPOKELEWA SHULENI** (itajazwa shuleni)

Tarehe aliyopokelewa shuleni …….. Kidato…….
Nambari ya Usajiri ……

KIAMBATANISHO NYOGEZA D:

NDUGU WATAKAO MTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI:

Mzazi/Mlezi wa ……. Kidato …… 20…….

Utaratibu wa shule unawaruhusu wazazi/walezi na ndugu wasiozidi wanne utakaowachagua wewe mwenyewe kufika shuleni kumjulia hali kijana wako. Wageni hupokelewa na Mwalimu wa zamu na kupokea maelezo na salamu za mzazi/mlezi au ndugu na kumfikishia mwanafunzi. Ni vyema wageni wafike saa za masomo kuweza kupata fursa ya kuonana na mwalimu wa darasa la mtoto ili kumjulia maendeleo yake ya kitaaluma.

NDUGU WA KWANZA

JINA……..

KAZI YAKE……

UHUSIANO NAYE…….

MAHALI ANAPOISHI…….

SIMU…….



NDUGU WA PILI

JINA……..

KAZI YAKE……

UHUSIANO NAYE…….

MAHALI ANAPOISHI…….

SIMU…….

NDUGU WA TATU

JINA……..

KAZI YAKE……

UHUSIANO NAYE…….

MAHALI ANAPOISHI…….

SIMU…….

NDUGU WA NNE

JINA……..

KAZI YAKE……

UHUSIANO NAYE…….

MAHALI ANAPOISHI…….

SIMU…….



Nimeelewa maelezo hayo hapo juu, Nina maoni yafuatayo (Eleza kama yapo):-

……

KIAMBATANISHO NYOGEZA E:

AHADI YA KUTII SHERIA /AMRI NA MAMLAKA YA SHULE:

1. Mimi Mwanafunzi……. Nimesoma kwa makini sheria zote za shule na nyongeza yake. Nimezielewa barabara na ninakubali kwa hiari yangu kuzitii na kuziheshimu. Nitafanya kazi na kusoma kwa bidii ili kujijengea msingi bora wa maisha yangu ya baadae ili kujiletea heshima na sifa yangu binafsi na shule yangu kwa ujumla.
   Ndimi mwanafunzi (Jina)
   ……
   Saini ……. Tarehe ……

2. Mimi …… Mzazi/Mlezi nimesoma sheria na taratibu za shule, Nimezielewa na mimi nakubali kijana wangu ajiunge/asijiunge na masomo katika shule hii.Nitahakikisha kukamilisha madeni yote ya shule kabla ya mwisho wa kila mwaka wa masomo wa kijana wangu, kumwezesha kuendelea na masomo bila bughudha yoyote.
   Ndimi Mzazi/Mlezi (Jina)
   …….

   Anuani ya kudumu:
   ……

   Saini …… Tarehe ……. Simu ……..

VITABU ANAVYOPASWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI

FV EGM

1. Ambros Odhiambo, Essentials for A-level Economics paper 1 & 2 Form 5 & 6 .
2. Essential for A - level pure mathematics form 5 & 6 by Telemu Majigwa
3. Mayombya P.L, Conceptual Advanced mathematics, Form V & VI
4. Zisti Kamili,The new physical geography paper 1
5. Zisti Kamili,Practical geography alive paper 1
6. Zisti Kamili,Human and economic geography paper 2

FV PCB

1. Taylor D.J, Green N.P.O, Stout G.W (2010). Biological Science (3rd Ed).
2. A – level physics by Chand.

3. A – level physics by Nelkon.
4. A – level chemistry by Chand.

FV PCM

1. A – level chemistry by Chand.
2. A – level physics by Chand.
3. A – level physics by Nelkon.
4. Essential for A - level pure mathematics form 5 & 6 by Telemu Majigwa
5. Mayombya P.L, Conceptual Advanced mathematics, Form V & VI



"KARIBU SANA KATIKA SHULE HII."